Matokeo ya kutozingatia Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani

SWAHILI

Novemba 2018

Australian Government
Department of Education and Training

NSW FAMILY DAY CARE ASSOCIATION INC.
since 1976

MKUSANYIKO WA TAARIFA ZA MWALIMU WA FAMILY DAY CARE:
Matokeo ya kutozingatia Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani

Kufuatilia uzingatiaji

Watoa huduma na vituo vya huduma za Family Day Care vilivyoidhinishwa husimamia Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto na Ruzuku ya Ziada ya Utunzaji wa Watoto kwa niaba ya familia chini ya Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani. Idara ya Elimu na Mafunzo ina mpango wa uadilifu wa kifedha ili kufuatilia uzingatiaji wa Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani kwa vituo vya kutoa huduma ya Family Day Care.

Lengo la mpango wa uadilifu wa kifedha ni kutoa hakikisho na uaminifu kuwa uwekezaji wa Serikali ya Australia katika mafunzo bora ya watoto wachanga na utunzaji wa watoto unatumiwa kwa namna sawa, kwa usawaziko na kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Vituo vya kutoa huduma na walimu wana jukumu la kuhakikisha ufadhili wa utunzaji wa watoto unasimamiwa Ipasavyo na unatumiwa kuzisaidia familia zinazostahiki ambazo zina gharama za kweli za utunzaji halisi wa watoto.

Idara ya Elimu na Mafunzo imejitolea kusaidia vituo vya kutoa huduma kuzuia makosa na kutozingatia kusitokee kwa mara ya kwanza. Aina tofauti za miongozo, hati za ukweli na nyenzo zingine za maelekezo zinapatikana ili kusaidia vituo vya kutoa huduma na walimu kupata ujuzi na ufahamu unaohitajika ili kusimamia malipo ya utunzaji wa watoto ipasavyo.

Pia kuna mamlaka na nyenzo zaidi za kutambua na kuchukua hatua dhidi ya kutozingatia na tabia ya ulaghai, ikiwemo kupitia Mfumo wa Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto.

Taarifa kutoka kwa mtu yeyote ambaye anajua shughuli za kutozingatia au ulaghai pia ni chanzo muhimu cha taarifa.

Ni nini hutokea ikiwa kituo chako cha kutoa huduma za Family Day Care hakizingatii Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani?

Watoa huduma na vituo vya kutoa huduma za Family Day Care wana jukumu la kuhakikisha usahihi wa ripoti zinazotolewa na walimu.

Walimu wanaweza pia kuwajibikia makosa ya uhalifu.

Ukweli wa mtu na historia yake ya kuzingatia sheria ni muhimu katika kuamua ufaafu wako wa kutunza watoto au kuendesha kituo cha kutoa huduma za kutunza watoto.

Watoa huduma na vituo vilivyoidhinishwa vya kutoa huduma za watoto wanaweza kuadhibiwa ikiwa hawatazingatia Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani. Adhabu zinazowezekana ni pamoja na:

- kurejeshwa kwa malipo yaliyozidi au ada za usaidizi wa utunzaji wa watoto zilizopokelewa kimakosa
- kuwekwa kwa masharti ya ziada kwa mtoa huduma au kituo cha kutoa huduma ili kudumisha idhini ya kusimamia Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto
- notisi za uvunjaji sheria
- kusitishwa kwa muda au kubatilishwa kwa idhini ya kusimamia Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto kwa niaba ya familia.

Katika hali fulani, kutozingatia pia ni kosa la uhalifu. Hii inaweza kupelekea adhabu kali, ikiwemo faini na/au kufungwa jela.

Idara ya Elimu na Mafunzo huchapisha taarifa kuhusiana na kuwekewa vikwazo, kusitishwa kwa muda au kubatilishwa kwa idhini ya watoa huduma na vituo vya kutoa huduma katika Sajili ya Hatua ya Utekelezaji wa Utunzaji wa Watoto: education.gov.au/child-care-enforcement-action-register. **education.gov.au/child-care-enforcement-action-register**.

Mabadiliko ya Sheria

Kumekuwa na mabadiliko kadhaa yaliyofanywa kwenye Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani ili kushughulikia kutozingatia hatari na uwezekano wa ulaghai kwa vituo vya kutoa huduma za Family Day Care. Mabadiliko hayo ni pamoja na:

- Vituo vilivyoidhinishwa vya kutoa huduma za Family Day Care ni lazima visitoe elimu na utunzaji katika jimbo au wilaya isipokuwa iwapo vimeidhinishwa katika jimbo hilo chini ya Sheria ya Kitaifa ya Huduma za Elimu na Utunzaji.
- Walimu wa Family Day Care hawawezi kupokea

  Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto kwa ajili ya watoto wao wenyewe kwa utunzaji uliotolewa na mwalimu mwingine kwa siku hio hio ambayo wanatoa huduma ya Family Day Care kwa watoto wa watu wengine, isipokuwa ikiwa hali maalum zilizobainishwa zinatumika (huu unaitwa 'ubadlishanaji wa watoto'). Mabadiliko mapya yanafafanua kanuni za ushahidi wa hati kwa kutohusishwa kwa elimu na kazi na yanahitaji vituo vya kutoa huduma za Family Day Care virekodi taarifa hiyo kwenye Sajili ya Hali Maalum Zilizobainishwa wakati wanapomtunza mtoto wa mwalimu.

- Ruzuku za utunzaji wa watoto hazilipwi kwa utunzaji wakati hakuna dhima halisi ya kulipa ada chini ya Makubaliano Yaliyoandikwa ya Uzingatiaji; utunzaji ambao aghalabu huwa usafiri; huduma ya Family Day Care iliyotolewa nyumbani kwa mtoto au pale ambapo mzazi yupo; au huduma ya Family Day Care au Utunzaji wa Nyumbani unaotolewa na mzazi au ndugu.
- Vituo vya kutoa huduma za Family Day Care ni lazima kila wakati viarifu Idara ya Elimu na Mafunzo wakati vinapofahamu kuwa wafanyakazi wao wakuu, mhudumu au mwalimu wao wa Family Day Care ameshtakiwa au kupatikana na kosa kubwa analoweza kushtakiwa, anafilisika au kukatazwa, kufanyiwa marekebisho au kubatilishiwa Kibali cha Kufanya Kazi na Watoto..
- Vigezo vyenye umakini zaidi vya ufaafu vinatumika kwa watu husika, ikiwemo wenye kutuma maombi ya kuidhinishwa kuwa watoa huduma au vituo vya kutoa huduma, vituo vya kutoa huduma vilivyoidhinishwa na watu fulani wanaohusiana nao.
- Vituo vya kutoa huduma za Family Day Care haviwezi kupokea tena Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto kwa niaba ya familia kwa watoto wenye umri wa miaka 13 au chini na wanaohudhuria shule ya upili au wenye umri wa miaka 14 au zaidi, isipokuwa ikiwa hawawezi kuachwa peke yao, na hakuna mtu mwingine mzima wa kuwachunga, na hali maalum iliyobainishwa ipo.
- Kuna vizuizi vipya vya kiasi cha utunzaji ambacho kinaweza kutolewa na walimu wa Family Day Care kwa jamaa. Watoto ambao ni mpwa, wa kike au kiume, binamu au mjukuu (akiwemo kitukuu) wa mwalimu wa Family Day Care ni lazima wawe chini ya asilimia 50 ya watoto ambao mwalimu anatoa utunzaji ndani ya wiki mbili zozote za Ruzuku ya Utunzaji wa Nyumbani. Uwiano huo hutumika kote kwa watoto wote wanaotunzwa katika wiki mbili zote, na sio tu kwa kipindi fulani kimoja.

Hii ina maana gani kwako?

Taarifa zaidi kuhusu maelezo mapya ya utunzaji wa watoto inapatikana kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Mafunzo katika: **www.education.gov.au/childcare**.

Mambo Muhimu

- Serikali hutoa usaidizi wa ada ya utunzaji wa watoto kwa familia zinazostahiki ambazo zinatumia huduma za Family Day Care chini ya Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani.
- Kituo chako cha kutoa huduma ya Family Day Care kina majukumu ya kisheria chini ya Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani.
- Kutoa rekodi za uwongo wa mahudhurio kwa kituo chako cha kutoa huduma ni kuvunja sheria.
- Kutoa huduma ya Family Day Care kwa watoto wa watu wengine katika siku sawia na ile ambayo watoto wako wanatumia huduma za Family Day Care, na kudai Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto, ni kinyume na sheria isipokuwa ikiwa hali maalum zilizobainishwa zinatumika.
- Kuripoti kuwa unamtunza mtoto wakati unamchukua tu kutoka shuleni na kumpeleka nyumbani ni kuvunja sheria.
- Kuilaghai Serikali kimakusudi ni uhalifu.
- Serikali ina njia nyingi za kugundua shughuli za kutozingatia sheria na za ulaghai.
- Matokeo ya kudai usaidizi wa ada ya utunzaji wa watoto kwa njia ya ulaghai yanaweza kuwa mabaya sana na yanaweza kujumuisha kusitishwa kwa muda au kubatilishwa kwa kibali cha mtoa huduma au kituo cha kutoa huduma, faini na/au kufungwa jela.

Mifano

This brochure has been produced in 11 languages: Amharic, Arabic, Assyrian, Dari, Dinka, French, Hazaragi, Nuer, Somali, Sudanese, and Swahili. To find the brochure in your language please go to **www.fdcsupport.org.au**

Kuripoti saa ulizotoa huduma ya Family Day Care ilhali wakati huo ulikuwa ng'ambo

Kituo cha kutoa huduma ya Family Day Care kiliwasilisha ripoti za vipindi za walimu 11 kwenye Mfumo wa Utunzaji wa Watoto wakati walikuwa ng'ambo. Wakati walipokuwa ng'ambo walimu hao waliendelea kutoa ripoti za mahudhurio kwa kituo chao cha kutoa huduma za Family Day Care kama ambao walikuwa wanawatunza watoto. Kituoa cha kutoa huduma za Family Day Care kilikuwa na wajibu wa kuhakikisha usahihi wa ripoti hizi za mahudhurio. Idara ya Uhamiaji na Ulinzi wa Mipaka hushiriki taarifa na mashirika mengine. Taarifa hii ilionyesha wakati walio hao waliondoka na wakati walirejelea tena Asutralia. Ushahidi huu, pamoja na data ya Mfumo wa Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto ambayo ilithibitisha kuwa utunzaji ulikuwa umeripotiwa kuwa ulifanyika, ulitolewa kwa Polisi wa Serikali Kuu ya Australia.

Matokeo: Kituo hicho cha kutoa huduma ya Family Day Care, ambacho kina wajibu wa kuhakikisha kuwa data inayowasilishwa ni sahihi, kiliwekewa vikwazo na kibali chake kubatilishwa chini ya Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani. Kituo hicho kilifungwa. Walimu hao walichunguzwa na Polisi wa Serikali Kuu ya Australia na kupatikana na kosa la ulaghai.

Kituo cha kutoa huduma ya Family Day Care ambapo 'ubadilishanaji wa mtoto' ulikuwa unafanyika

Baada ya 'ubadilishanaji wa mtoto' kupigwa marufuku, walimu kadhaa katika kituo fulani cha kutoa huduma ya Family Day Care waliendelea kufanya hivyo. Idara ya Elimu na Mafunzo iliwasiliana na kituo hicho na kukiomba kitoe sajili na hati ya kuonyesha kuwa 'ubadilishanaji wa mtoto' ulikuwa unatokea tu kulingana na masharti yanayokubaliwa chini ya Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani.

Matokeo: Haikuchukua muda mrefu kabla ya Idara ya Elimu na Mafunzo kugundua kuwa ushahidi uliotolewa na kituo hicho ulionyesha kuwa walikuwa wanavunja Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani. Kituo hicho kiliadhibiwa na kibali chake kubatilishwa. Kwa sababu kituo hicho kilikuwa kimevunja sheria kwa 'kubadilishana watoto' kinyume na sheria, kesi hiyo iliwasilishwa kwa Polisi wa Serikali Kuu ya Australia.

Utunzaji unaohusisha sehemu kubwa ya usafiri

Mwalimu wa Family Day Care anamchukua mtoto kutoka shuleni saa 9.30 adhuhuri kila siku na kumsafirisha kwenda nyumbani kwa mtoto huyo saa 10.15 alasiri. Mwalimu huyo anaripoti nyakati hizi kwenye ripoti ya mahudhurio kama kwamba alikuwa anamtunza mtoto huyo. Huduma ya Family Day Care iliripoti mahudhurio ya utunzaji wa mtoto huyo katika Mfumo wa Utunzaji wa Watoto.

Matokeo: Huduma ya Family Day Care haipaswi kamwe kuripoti utunzaji ambao unahusisha hasa usafiri pekee. Wakati kituo hicho cha huduma kilipowasilisha data hiyo kama utunzaji, walikiuka masharti yanayowaidhinisha kuendelea kuwa na kibali cha utunzaji wa watoto. Kukosa kuzingatia kanuni hii kulipelekea kusitishwa kwa muda mara moja kwa kibali cha kituo hicho kulingana na Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani.

Kumbuka: *Hii haiathiri mipangilio ambayo inahusisha utoaji wa huduma ya usafiri kwa watoto kama sehemu ya utunzaji wa mtoto. Hivyo ni kusema kuwa, usafiri unapaswa kuwa kipengele tu cha kipindi cha utunzaji wa mtoto lakini si sehemu kubwa au yote ya utunzaji.*

Utunzaji Unaotolewa na Jamaale

Mwalimu wa Family Day Care alifanya kazi kwa siku nne kwa wiki na kutunza watoto wawili wasio jamaa wake ambao hawajafikisha umri wa kwenda shuleni na wanaokuja kila siku kwa siku nne kwa wiki. Mwalimu huyo aliendelea kumtunza mpwa wake wa kiume wa umri wa miaka minne na mpwa wake wa kike wa umri wa mwaka mmoja kwa siku mbili kwa wiki. Hii ni sawa na uwiano wa asilimia 50 ya utunzaji unaotolewa kwa jamaa ndani ya wiki mbili. Hii ina maana kuwa mwalimu huyo alizidi uwiano mpya wa chini ya asilimia 50 ya utunzaji unaotolewa kwa jamaa ndani ya wiki mbili.

Matokeo: Kituo hicho cha Family Day Care kilivunja masharti ya kuendelea kuwa na kibali cha kutoa huduma ya utunzaji kwa kukosa kuhakikisha kuwa chini ya asilimia 50 ya watoto kinachotunza ndani ya wiki mbili ni jamaa wa mwalimu. Hii ilipelekea kusitishwa kwa muda kwa kibali cha kituo hicho chini ya Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani. Mwalimu huyo alihitaji kutunza angalau mtoto mmoja zaidi asiye jamaa kwa angalau siku moja ya wiki mbili hizo ili kuendelea kutunza mpwa wake wa kike na wa kiume.

Novemba 2018

Amharic በራስዎ ቋንቋ በራሪ ወረቀት ለማግኘት **www.fdcsupport.org.au**. ድረ ገጽን ይመልከቱ

Arabic لإيجاد الكتيب بلغتك، يُرجى تصفح موقع الويب **www.fdcsupport.org.au**.

Assyrian ܠܡܫܟܚܘܬܐ ܦܢܝܬܐ ܒܠܫܢܘܟ، ܒܝ ܒܥܝܐ ܣܝܪ ܠܘܒ ܕܣܝܬ ܕܐܝܢܛܪܢܝܬ **www.fdcsupport.org.au**.

Dari برای دریافت جزوه به زبان خودتان، لطفاً به ویبسایت **www.fdcsupport.org.au** مراجعه کنید.

Dinka Të kɔɔr yin kitap në thoŋdu kitam tɔ̈ wëlthin ke yin lɔ në **www.fdcsupport.org.au**.

French Pour trouver la brochure dans votre langue, veuillez visiter le site **www.fdcsupport.org.au**.

Nuer Kɛ ɣöö bi ŋäc jiek rɛy warɛgakä/ kiɛ majalɛ kɛ thuok du, göa ɛ ɛn ɣöö bi wä kä **www.fdcsupport.org.au**.

Hazaragi برای دریافت این بروشور به زبان خود تان، لطفاً به ویب سایت **www.fdcsupport.org.au** مراجعه کنید.

Somali Si aad ugu heshid buugyaraha luuqadaada fadlan booqo **www.fdcsupport.org.au**.

Sudanese لإيجاد الكتيب بلغتك، الرجاء تصفح موقع **www.fdcsupport.org.au**.

Swahili Ili kupata brosha hiyo kwa lugha yako tafadhali tembelea tovuti **www.fdcsupport.org.au**.

Find out more by going to:

- **www.education.gov.au/child-care-provider-handbook-0**
- **www.education.gov.au/compliance**
- **www.education.gov.au/child-care-providers**
- **www.fdcsupport.org.au**
- **www.fdca.com.au**
- **www.acecqa.gov.au**

Or by going to the website of your Family Day Care service or to other information they have provided you such as handbooks or induction manuals.

Australian Government
Department of Education and Training

NSW FAMILY DAY CARE ASSOCIATION INC.